



SYRACUSE CITY SCHOOL DISTRICT

Jaime Alicea, Msimamizi wa Shule

Office of Teaching and Learning

Laura Kelley, Chief Academic Officer

20 Machi, 2020

Kwa Familia za Shule ya Upili,

Tumekuwa tukijitahidi kuhakikisha kuwa wanafunzi wetu wataweza kuendelea kuwa na shughuli wakati huu ambao hawawezi kuenda shuleni. Tumeunda rasilimali kwenye ngazi ya wilaya na tunajua kuwa shule binafsi na walimu wa watoto wenu pia wamekuwa wakiwapa watoto wenu rasilimali ili kushiriki katika masomo nyumbani.

Ili kuufanya mchakato huu kuwa bayana na rahisi iwezekanavyo, tumeunda sampuli ya ratiba kwa watoto walio kwenye madaraja ya 9-12. Ratiba hii itatoa njia ambayo inaunga mkono masomo endelevu, kuendeleza afya ya mhemko na kuhimiza shughuli za kujenga mwili na tabia za siha njema. Ikiwa shule au mwalimu wa mtoto wako tayari ametoa ratiba ambayo ni tofauti, au ikiwa una ile inayoifaa familia yako, tafadhali kuwa huru kutumia hiyo badala yake.

Kuhusu muda wa elimu, **tafadhali kipe kipaumbele chochote ambacho kilitumwa nyumbani kutoka kwa mwalimu wa darasa au shule ya mtoto wako.** Ikiwa shughuli hizo zitakwisha, pia unaweza kufikia rasilimali zifuatazo zilizotolewa na District Office. Unaweza kuzipata kwenye www.syracusecityschools.com/coronavirus.

Pia kuna baadhi ya chaguo zinazotolewa na WCNY/PBS. Tafadhali tazama tovuti ya wilaya kwa ratiba ya vipindi vya elimu iliyopo kwenye WCNY PBS (Idhaa: Kupitia Hewani 24.1, Spectrum 1221, Verizon FiOS 11/511, DirecTV 24.1, na DISH 24). Nyingine zitakuja baada ya wiki chache; endelea kuangalia tovuti ya wilaya kwa taarifa zaidi zinapoingia.

Ikiwa wewe ni mhudumu wa afya anayehitaji malezi ya mtoto wakati wa shule kufungwa, tafadhali piga simu (315) 446-1220 kwa taarifa na usaidizi.

Kila la heri,

Laura Kelley

Sampuli ya Masomo kutoka Shule ya Upili ya Ratiba ya Nyumbani

Saa	Shughuli zinazopendekezwa
9:00-12:00	<ul style="list-style-type: none"> • Pata kifunguakinywa na ujitayarisha kwa siku (oga, vaa nguo, piga mswaki, n.k.) • Dakika 120 za muda wa elimu (kutumia rasilimali ulizopewa na shule au wilaya; kuwa huru kugawa kwa mafungu ya dakika 30-60) <ul style="list-style-type: none"> ○ Maudhui/Kozi ya Dijitali

	<ul style="list-style-type: none"> ○ Kazi ya Karatasi/Penseli ○ Kusoma na/au Kuandika ● Dakika 30 za shughuli za kimwili ● Dakika 30 za mapumziko
Saa ya Chamcha!	
12:30-3:00	<ul style="list-style-type: none"> ● Dakika 90 za muda wa elimu (kutumia rasilimali ulizopewa na shule au wilaya) <ul style="list-style-type: none"> ○ Maudhui/Kozi ya Dijitali ○ Kazi ya Karatasi/Penseli ○ Kusoma na/au Kuandika ● Dakika 30 za shughuli za kimwili ● Dakika 30 za mapumziko